# Uchunguzi wa saratani ya koloni kwa kutumia kipimo cha Cologuard®

## Kipimo cha Cologuard kinashughulikiwa na watoa huduma wengi wa matibabu na makampuni mengi makubwa ya bima.

**$0** Wagonjwa wengi walio na bima hulipia **$0** kwa kipimo cha Cologuard[1]*

**96%** Nchini kote, zaidi ya asilimia **96%** ya wagonjwa wa Cologuard hawana gharama inayotoka mfukono kwa ajili ya uchunguzi[1]*

**Jifunze zaidi** kwenye **Cologuard.com/insurance** au piga **1-844-870-8870.** Tunaweza kukusaidia kuuliza kampuni yako ya bima maswali sahihi.

Bima nyingi **hugharamia colonoscopy ya ufuatiliaji** baada ya uchunguzi chanya wa Cologuard.[2,3†]

**Video ya Jinsi Ya Kutumia: Cologuard.com/tumia**

## Kipimo cha Cologuard ni rahisi kutumia ukiwa nyumbani

**Maagizo ya Kina yapo kwenye Sanduku la Cologuard**

### 1 KAA



- Tumia kipimo cha Cologuard ukiwa tayari.
- Weka chombo chako cheupe cha Sampuli juu ya choo.
- Kaa kwenye choo.

### 2 KWAGUA



- Kunya kwenye hicho chombo cheupe cha sampuli.
- Kwagua kinyesi chako kwa kijiti na urudishe ndani ya bomba kutoka kwenye seti.

### 3 LOWESHA NA UFUNGE



- Jaza chombo cha sampuli na kihifadhi cha kioevu.
- Funga kile chombo kikubwa kilicho na sampuli yako ndani.

### 4 WEKA LEBO NA USAFIRISHE



- Jaza lebo zote mbili.
- Rejesha seti hii kwa Exact Sciences kupitia UPS®.

**Rudisha sampuli yako bila malipo**

1. Panga uchukuzi wa UPS kwenye **Cologuard.com/UPS** au piga **1-844-870-8870**
2. Peleka seti yako kwa UPS. Tafuta maduka ya karibu na saa za kuchukuliwa kwa **Cologuard.com/UPS**

*Makadirio ya hivi majuzi ya Exact Sciences kulingana na malipo ya kihistoria ya mgonjwa.
†Kwa wagonjwa wengi, hii itaanza kutumika tarehe 1 January 2023, na haitumiki kwa mipango ya kibiashara yenye hadhi iliyoondolewa.[2,3]

# **Matokeo** ya kipimo chako cha Cologuard®

**Mtoa huduma wako wa afya anapaswa kupata matokeo yako ndani ya siku 8-10 baada ya Exact Sciences kupokea sampuli yako.**



Kipimo cha Cologuard kinatafuta **DNA iliyobadilishwa** na **damu** (dalili za saratani) kwenye kinyesi chako[4]

− Matokeo hasi inamaanisha kuwa kipimo cha Cologuard hakikupata dalili za saratani. Una uwezekano mkubwa huna saratani ya utumbo mpana.[4]

\+ Matokeo chanya inamaanisha kuwa kipimo cha Cologuard kiligundua dalili za saratani. Matokeo chanya **haimaanishi** kuwa una saratani.[4] Panga miadi ya kufuatilia na mtoa huduma wako wa afya.

Baadhi ya watu hupata matokeo chanya na hasi ya uongo (yasiyo sahihi). Daima muulize mtoa huduma wako wa afya kuhusu hatua zinazofuata za ukaguzi.[4]

Pata maelezo zaidi na video kwenye:
**Cologuard.com/UnderstandingResults**

## Dalili naTaarifa Muhimu za Hatari

Kipimo cha Cologuard kinakusudiwa kuwakagua watu wazima walio na umri wa miaka 45 na zaidi walio katika hatari ya wastani ya saratani ya utumbo mpana kwa kugundua alama fulani za DNA na damu kwenye kinyesi. Usitumie ikiwa umekuwa na adenomas, una ugonjwa wa kuvimba matumbo na syndromes fulani za urithi, au historia ya kibinafsi au ya familia ya saratani ya utumbo mpana. Kipimo cha Cologuard si mbadala wa colonoscopy katika wagonjwa walio katika hatari kubwa. Utendaji wa kipimo cha Cologuard kwa watu wazima wenye umri wa 45-49 unakadiriwa kulingana na utafiti mkubwa wa kimatibabu wa wagonjwa wenye umri wa miaka 50 na zaidi.

Matokeo ya kipimo cha Cologuard yanapaswa kutafsiriwa kwa tahadhari. Matokeo chanya ya kipimo hayathibitishi uwepo wa saratani. Wagonjwa walio na matokeo chanya wanapaswa kutumwa kwa colonoscopy. Matokeo hasi ya kipimo hayathibitishi kutokuwepo kwa saratani. Wagonjwa walio na matokeo hasi ya kipimo wanapaswa kujadiliana na daktari wao wanapohitaji kupimwa tena. Matokeo chanya ya uongo na matokeo hasi ya uongo yanaweza kutokea. Katika utafiti wa kimatibabu, 13% ya watu wasio na saratani walipata matokeo chanya (chanya ya uongo) na 8% ya watu walio na saratani walipata matokeo hasi (hasi ya uongo). Rx only

**Marejeleo:** **1.** Internal Data on File. Exact Sciences. **2.** FAQs about Affordable Care Act Implementation Part 51, Families First Coronavirus Response Act and Coronavirus Aid, Relief, and Economic Security Act Implementation. US Department of Health & Human Services. Published January 10, 2022. Accessed May 22, 2025. https://www.hhs.gov/guidance/document/faqs-about-affordable-care-act-implementation-part-51. **3.** CMS. Calendar year (CY) 2023 Medicare physician fee schedule final rule. Published November 1, 2022. Accessed May 22, 2025. https://www.cms.gov/newsroom/fact-sheets/calendar-year-cy-2023-medicare-physicianfee-schedule-final-rule. **4.** Exact Sciences. 2024. Cologuard Patient Brochure.

EXACT SCIENCES CORPORATION | 5505 Endeavor Lane, Madison, WI 53719
ExactSciences.com | ExactLabs.com | 1-844-870-8870

Cologuard na Exact Sciences ni alama za biashara zilizosajiliwa za Exact Sciences Corporation.
Alama nyingine zote za biashara ni mali ya wamiliki husika.
© 2025 Exact Sciences Corporation. Haki zote zimehifadhiwa. M-US-CG-06571_Swahili_May 2025

cologuard® by EXACT SCIENCES